

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



## OFISI YA RAIS

MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA  
 AHADI YA UADILIFU KWA WATUMISHI WA UMMA  
 (Kwa Utumishi wa Umma uliotukuka)

Kwa kutambua dhamira ya kuufanya utumishi wa umma kuwa wenye ufanisi na kuheshimika kutokana na watumishi kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma, Na. 8 ya mwaka 2002, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na Kanuni za Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma za mwaka 2005 pamoja na kuwa na mwenendo unaozingatia maadili; Mimi..... ninaahidi kwa umma kwamba:

1. Nitakuwa Mzalendo kwa nchi yangu na mtii kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
2. Nitahudumia umma na watumishi wenzangu kwa heshima;
3. Nitatimiza wajibu wangu wa kutoa huduma bora kwa umma;
4. Nitatoa huduma bora kwa usawa kwa watu wote na kutofanya ubaguzi kwa misingi ya dini, siasa, kabila, udugu, ukanda, jinsia, urafiki au hali ya mtu;
5. Sitaomba, kushawishi, kutoa wala kupokea rushwa;
6. Sitaomba, kutoa wala kupokea zawadi au fadhila za kiuchumi au za kjsiasa au kijamii zisizoruhusiwa na Sheria;
7. Sitatumia madaraka yangu kwa manufaa binafsi, ya ndugu, rafiki au jamaa zangu;
8. Nitatekeleza wajibu wangu kwa kufuata Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbali mbali ya Utumishi wa Umma;
9. Nitafanya kazi kwa bidii na nidhamu ya hali ya juu;
10. Nitālinda na kutumia rasilimali za umma kwa manufaa ya umma;
11. Nitaepuka tabia ambayo inavunja heshima ya utumishi wa umma hata ninapokuwa nje ya mahali pa kazi;
12. Sitatoa siri za Serikali au za mteja kwa watu wasiohusika isipokuwa kwa maslahi ya umma;
13. Nitajiepusha na mgongano wa maslahi na pale utakapojitokeza nitaotatua kwa maslahi ya umma.

Tamko: Ninakiri kwamba nimeisoma Hati hii ya Ahadi ya Uadilifu kabla ya kuweka sahihi. Ninakubaliana na kutambua kwamba masharti yaliyo katika Hati hii ni ya kimaadili na kisheria na ninawajibika kuyatekeleza. Ninaelewa kwamba ukiukwaji wa masharti hayo ni ukiukwaji wa maadili na masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria ya Kudhibiti Mgongano wa Maslahi, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma, Kanuni za Maadili ya Kitaaluma na kwamba hatua za kinidhamu na kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi yangu iwapo nitakiuka masharti hayo.

.....  
JINA.....  
CHEO.....  
SAINI.....  
TAREHE.....  
MTENDAJI MKUU WA TAASISI.....  
TAASISI.....  
SAINI.....  
TAREHE